

GENDA SECONDARY SCHOOL

S. L. P 286

MBULU - MANYARA



WANAFUNZI MAABARA



WANAFUNZI WA A - LEVEL



WANAFUNZI MAABARA



PICHA YA WAALIMU NA WATUMISHI



WANAFUNZI WA O - LEVEL



KWA MAWASILIANO

Mkuu wa Shule - 0786 595 759. - Makamu mkuu wa Shule - 0686 907 337.

Mwandamizi taaluma - 0784 804814. - Msajili wa kidato cha kwanza 2025 - 0786 384 969.

Email. gendasecshool2010@gmail.com-Website: www.genda1998.com

SHULE YA SEKONDARI GENDA.

Shule ya Sekondari Genda imesajiliwa na Wizara ya Elimu tarehe 14/05/2010 kwa namba S. 4329 na kupewa namba ya usajili baraza la mtihani Tanzania namba S. 4351.

Shule ipo Mkoa wa Manyara Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Hii ni shule ya binafsi (Private),

Shule ni ya mchanganyiko (wasichana na wavulana) kidato cha Kwanza hadi cha Sita na watoto wote wanaishi bweni.

TAALUMA.

Shule hii ni miongoni mwa shule bora sana Tanzania kwani wanafunzi wake hufaulu kwa daraja la I-III kwa 99%.

Tazama matokeo ya miaka mitatu ya hivi karibuni kidato cha Nne.

MWAKA	I	II	III	IV	O
2020	50	64	08	00	00
2021	66	66	4	00	00
2022	42	82	15	00	00
2023	55	65	25	03	00

GHARAMA (ADA YA SHULE)

Ada yetu ni nafuu sana na inalipwa kwa awamu kama chati inavyoonyesha hapo chini na hakuna michango mingine.

JANUARY	APRIL	JULAI	SEPTEMBER
400,000/=	400,000/=	400,000/=	400,000/=

Jumla ya ada ni 1,600,000/= kwa mwaka katika ada hiyo mtoto atapata huduma zote shuleni na matibabu ngazi ya Shule hadi Hospitali ya Mji wa Mbulu bila mzazi kugharamia.

pia atapewa godoro Shuleni katika ada hiyo.

MWONGOZO WA SARE

Maelekezo ya sare yatakuwa katika fomu ya kujiunga na shule itakayotolewa pale atakapochaguliwa kujiunga na shule mwaka 2025

MALEZI.

Watoto wa Dini zote wanapokelewa na wanalelewa kulingana na imani zao na kukuzwa katika misingi ya umoja na mshikamano.

Ewe mzazi usihangaikie kutafuta shule, Mlete mwanao Genda Sekondari kwani ipo kutimiza ndoto ya kila mzazi kwa mtoto wake.

NAFASI ZA MASOMO.

Shule inatangaza nafasi ya kozi ya maandalizi ya kidato cha kwanza 2024 (Pre Form One) Mapokezi/Masomo yataanza tarehe 25/09-10/10/2024 na kuhitimishwa tarehe 07/12/2024.

Gharama ya kozi hii ni Tsh. 250,000/= na italipwa kwa awamu mbili awamu ya kwanza Tshs 150,000/= siku ya kuripoti shuleni na awamu ya pili Tshs 100,000/= italipwa tarehe 24/11/2024.

Nafasi zilizopo ni za kuishi bweni tu, na watoto watapata huduma zote shuleni kwa gharama iliyoainishwa hapo juu.

Mtihani wa kujiunga na shule kwa kidato cha kwanza mwaka 2025 utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 29/11/2024 saa mbili kamili asubuhi shuleni Genda Sekondari.

Gharama za mtihani ni Tshs. 30,000/= itawahusu wale ambao hawajashiriki kozi ya Pre Form One.

VIFAA ATAKAVYOKUJA NAVYO WAKATI WA KUANZA KOZI YA PRE FORM ONE.

1. Traksuti ya rangi ya Kijivu moja
2. Sare zake za shule ya msingi au sketi/Suruahi nyeusi moja, shati ya blue/nyeupe moja.
3. Sweta moja ya baridi nyeusi au blue isiwe na kofia
4. Viatu vyeusi pea moja na malapa
5. Daftari ndogo msomi 10 na begi la daftari.
6. Blanketi moja na shuka mbili Pink wasichana, Blue Wavulana
7. Taulo au kanga kwa wasichana
8. Sabuni ya kuogea na kufulia zinazotosha miezi miwili
9. Dawa ya meno, mafuta ya kupaka na kiwi ya viatu

VIFAA ATAKAVYOPEWA SHULENI

Ndoo ndogo, T - sheti yenye nembo ya shule, godoro moja na vyombo vya kulia chakula.

NB. Ukija na fedha vitu hivyo vyote unaweza kupata shuleni au Mbulu Mjini. Vifaa hivi hasa Traksuti, Blanketi hautarudia kununua iwapo atajiunga na Genda Sekondari.